

جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية المجالس بالزلفي
مشروع تَعْلُمُ الْإِسْلَام – أحكام الطهارة - سواحيلي

Samo la 7

الدرس السابع

**KUTAYAMAMU (KUJITWAHARISHA KWA KUTUMIA
MCHANGA)**

Inafaa kutayamamu ukiwa mjini au ukiwa safari, kutayamamu inachukua nafasi ya ushu au kuoga itakapopatikanwa sababu mionganoni mwa sababu zifuatazo;

1. Kukosekana maji, iwapo yatapatikana maji lakini hayatoshi kujitwaharishia, lakini inatakikana afanye juhudzi za kuyatafuta kwanza, akiyakosa atatayamamu, au maji yanakuwa karibu yake isipokuwa anaogaopea nafsi yake, mali yake kutohana na maudhi ya watu wabaya, asije akadhurika pindi akitoka nje kuyatafuta maji, hapo atatayamamu.
2. Ikiwa moja ya kiungo cha kutawadha kinajeraha, atakiosha na maji, na ikiwa kujiosha kwake kunaleta athari basi atakipangusa na unyevu nyevu wa maji juu yake, ataulowesha mkono wake kisha ataupitisha juu ya hicho kiungo kilichokwu na jeraha, na ikiwa kupangusa kunaathiri basi ataviosha baadhi ya viungo kisha kile chenyé jeraha atakitayamamisha kwa mchanga.
3. Ikiwa maji ni ya baridi sana au hali ya hewa ni ya baridi sana na anaechelea kupata madhara pindi akitawadha kwa maji atatayamamu.
4. Akiwa maji anayo, lakini anayahitaja kwa ajili ya kunywa au kupiklia basi atatayamamu.

NAMNA YA KUTAYAMAMU.

1. Atanuia moyoni mwake. (Kutia nia).
2. Atapiga viganja vyake viwili ardhini mara moja kisha atapangusa uso wake na kupangusa kwa kutumia matumbo ya vidole vyake, matumbo ya vidole vya mkono wa kushoto yatapangusa juu ya kiganja cha mkono wa kulia, na matumbo ya vidole vya mkono wa kulia yatapangusa juu ya kiganja cha mkono wa kushoto.

Inatenguka kutayamamu kwa yale yote yanayo tengua udhu, kama vile inatenguka kwa kupatikana maji kwa yule aliyekosa maji kabla ya swala au katikati ya swala, au atakaepata maji baada ya kumaliza kuswali, swala yake ni sahihi wala hawezi kuirudia swala yake.